**BARAZA LA WAWAKILISHI – ZANZIBAR**

**ORODHA YA SHUGHULI ZA LEO**

**<u>BARAZA LA KUMI LA WAWAKILISHI</u>**

**<u>MKUTANO WA TATU</u>**

**<u>Kikao cha Pili – Tarehe 06 Mei, 2021.</u>**
Kikao Kitaanza Saa 3.00 (Tatu) Asubuhi
na Dua itasomwa.

## I. <u>HATI ZA KUWASILISHA MEZANI:</u>

**<u>Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais</u>:**

Hotuba ya Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2021/2022.

**<u>Mwenyekiti wa Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa:</u>**

Hotuba ya Maoni ya Kamati ya Kusimamia Ofisi za Viongozi Wakuu wa Kitaifa kuhusu Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa Mwaka 2021/2022.

## II. **MASWALI:**

**Ofisi ya Makamo wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

42. MHESHIMIWA MACHANO OTHMAN SAID (Jimbo la Mfenesini) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Afisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera na Uratibu wa Baraza la Wawakilishi:

Kwa muda mrefu Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) imekuwa ikifadhili miradi ya maendeleo ya kimiundombinu katika nchi wanachama wa Jumuiya hiyo. Kwa vile Zanzibar ni sehemu ya Tanzania na kwa kuwa Tanzania nayo inafadhiliwa kwa miradi hiyo ikiwemo ya ujenzi wa barabara na reli ambazo zitaiunganisha Tanzania na nchi nyengine.

(a) Kwa kuwa Zanzibar kwa kipindi kirefu iliahidiwa kusaidiwa miradi ya ujenzi wa kiwanja cha ndege cha Zanzibar na mradi wa usafiri wa bahari. Je ni hatua gani zimeshachukuliwa hadi sasa.

(b) Kwa kipindi chote tokea kuanzishwa tena Jumuiya ya Afrika Mashariki hadi sasa. Je, Zanzibar imepata mradi gani.

**Ofisi ya Makamo wa Kwanza wa Rais:**

116. MHESHIMIWA SULUBU KIDONGO AMOUR (Jimbo la Mkwajuni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:

Wananchi wa Mkwajuni wanaojishughulisha na kilimo cha mwani wamekuwa wakisumbuliwa kwa muda miaka kumi sasa kutokana na wawekezaji hao wa Hoteli katika eneo hilo kulaza mabomba yenye maji yenye kemikali za sumu ya mabwawa ya hoteli hizo kuelekea baharini (*Swimming pool*). Hali hii huharibu mazingira ya bahari na kuuwa zao la mwani.

(a) Je, Wizara inalifahamu tatizo hilo.

(b) Je, wawekezaji hao wanawatazama vipi wananchi ambao wanapata riziki zao kupitia kilimo cha mwani katika maeneo hayo.

**Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:**

55. MHESHIMIWA YAHYA RASHID ABDULLA (Jimbo la Kwahani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Fedha na Mipango:

Kumekuwa na tatizo la kuchelewa kwa fedha za matumizi mengineyo (Other Charge) zinazopelekwa Manispaa na Halmashauri.

(a) Je, tatizo hili linasababishwa na nini.

(b) Kwa kuwa nauli za watumishi zinatolewa kupitia fedha za kwa fedha za matumizi mengineyo (Other Charge), Je, Serikali haioni kwamba ucheleweshaji huo unapelekea wafanyakazi kuchelewa kazini kufika kwa wakati.

(c) Ni kwa nini nauli za watumishi hao zisiingizwe katika mishahara yao.

**Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:**

29. MHESHIMIWA HASSAN HAMAD OMAR (Jimbo la Kojani) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Katiba, Sheria, Utumishi na Utawala Bora:

Suala la Tahfidh Qur-ani kwa sasa ni taaluma muhimu kitaifa na kimataifa. Serikali za nchi mbali mbali duniani huandaa mashindano ya kitaifa na kimataifa kwa ajili ya kukuza vipaji na kuendeleza taaluma hiyo.

(a) Je, Serikali imeandaa utaratibu gani katika kuinua vipaji vya watoto wetu.

(b) Ni kwa kiasi gani Serikali huzisaidia madrasa katika kuandaa mashindano hayo katika ngazi za kijiji, shehia na mikoa.

**Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:**

4. MHESHIMIWA SHAABAN ALI OTHMAN (Jimbo la Mpendae) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Nchi, Ofisi ya Rais, Kazi, Uchumi na Uwekezaji:

Serikali imekuwa ikifanya jitihada kubwa za kuvutia wawekezaji nchini, lakini licha ya jitihada hizo, suala la upatikanaji wa maeneo kwa uwekezaji imekuwa ni changamoto.

(a) Je, Serikali ina mpango gani wa kuyarudisha maeneo muhimu ya uwekezaji yanayodhibitiwa kwa muda mrefu bila ya kuendelezwa na wawekezaji wasio wazalendo.

.

(b) Je, Serikali inatambua kuwa wapo baadhi ya wawekezaji waliidanganya Serikali kwa muda mrefu sasa kupitia andiko la mradi na hatimaye kupewa ardhi kubwa na hadi sasa hawajaiendeleza kama ilivyokusudiwa.

**Wizara ya Biashara na Maendeleo ya Viwanda:**

31. MHESHIMIWA Shamata Shaame Khamis (Jimbo la Micheweni) - Atamuuliza Mheshimiwa Waziri wa Biashara na Maendeleo ya Viwanda:

Kumekuwa na malalamiko kwa baadhi ya wananchi wanaofuatilia mwenendo wa bei za bidhaa mbali mbali kuhusu kuwepo kwa utofauti wa bei baina na visiwa vya Pemba na Unguja.

(a) Je, Wizara yako inalifahamu hilo.

(b) Ikiwa inalifahamu, ni sababu gani zinazopelekea kuwepo kwa tofauti hizo.

(c) Je, Serikali itachukua hatua gani juu ya jambo hili ili kuwapunguzia mzigo wakaazi wa kisiwa cha Pemba.

**III. HOJA ZA SERIKALI:**

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Pili wa Rais, Sera, Uratibu na Baraza la Wawakilishi kwa mwaka 2021/2022.

**Waziri wa Nchi, Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais:**

Kwamba Baraza hili lijadili Makusudio na Shabaha zilizomo katika Makadirio ya Mapato na Matumizi ya Ofisi ya Makamu wa Kwanza wa Rais kwa mwaka 2021/2022.

**Zanzibar,** **(Raya Issa Msellem)**
**6 Mei, 2021.** **KATIBU WA BARAZA.**